

Ukanushi katika vitenzi vya lugha ya kibena: Msingi wa kimofosintaksia

Irene Edward Mbunda

Uzamili ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Institute of Kiswahili Studies, 2012

Utafiti huu unaliusu utokeaji wa mofimu za ukunnslii kalika vitenzi vya lugha ya Kibena. Data iliyojadiliwa katika utafiti huu imekusanywa kutoka kalika vijiji vitatu ambavyo ni Mlwango, Ilunda na Kichiwa, Vijiji hivi vipo kalika wilaya ya Njombe, mkoani Njoinbe. Data msingi na data fuatizi /imetumika katika utafiti huu. Data msingi ilikusanywa uwandani, wakati data fuati/i ilikusanywa kutoka maktabani. Utafiti huu umegawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza imeonesha suala lililochunguzwa katika utafiti huu pamoja na mipaka yake. Sura ya pili imeonesha msingi wa nadharia ya Umbo Upeo iliyoasisiwa na Prince na Smolensky (1993), Nadharia hii imetumika kama mwongozo wa uchambuzi wa data iliyokusanywa. Vilevile machapisho mbalimbali yanayoelezea juu ya mofimu za ukanushi katika vitenzi vya lugha mbalimbali za Kibantu yameoneshwa katika sura ya pili. Sura ya tatu inaonesha mbinu zilizotumiwa na mtafiti katika kukusanya data ya utafiti ambayo imechambuliwa na kufafanuliwa katika utafiti huu. Mbinu ya ushuhudiaji, hojaji na usaili zimeelezwa kuwa zimetumika katika kukusanya data uwandani. Mbinu ya kusoma na kunukuu imetumika kukusanya data maktabani. Sura ya nne imeonesha uchambuzi wa data ulivyofanyika katika utafiti huu kwa kuzingatia masharti zuizi yanayozuia mofimu za ukanushi kujitokeza katika ruwaza zisizo kubalifu katika lugha ya Kibena. Uzingatiaji wa masharti zuizi hayo unatokana na mwongozo wa nadharia ya Umbo Upeo iliyo na madai ya msingi kuwa maumbo mbalimbali ya lugha hutokana na masharti zuizi yaliyopo. Hivyo mofimu za ukanushi zimebainishwa kujitokeza kulingana na masharti zuizi ya utokeaji wa mofimu hizo katika lugha ya Kibena. Sura ya tano imeonesha matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo ya tafiti fuatishi. Data ya utafiti imebaini kuwepo kwa mofimu nne za ukanushi katika lugha ya Kibena. Mofimu hizo zimeoneshwa kuwa hujitokeza mwanzoni mwa vitenzi vinavyokanushwa. Vilevile data ya utafiti imebaini kuwa lugha ya Kibena haina tabia ya kupachika mofimu za ukanushi zaidi ya moja katika kitenzi kimoja.